

HALMASHAURI YA MJI HANDENI

Simu	027-2641807
Fax	027-2641824
Kumbu yako	
Kumbu yetu	MED/HD/350/120



Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji,
S.L.P. 51,
Handeni, Tanga,

TANZANIA.

13/09/2019

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji Handeni kwa kushirikiana na shirika la AMREF anawatangazia Wananchi wote wenye sifa za kuomba nafasi za kazi za muda mfupi (Mkataba) kwa kada mbalimbali kama ifuatavyo:-

- I. Kazi : **Mteknolojia Maabara (1)**
Eneo la kazi: **Handeni – Tanga**
Atawajibika kwa :**Mkuu wa kitengo cha huduma ya tiba na matunzo (CTC)**

MAELEZO YA KAZI

Kazi ya Mteknolojia maabara ni kwa ajili ya kuimarisha ubora wa huduma za upimaji wa virusi vya Ukimwi na ufuatiliaji wa wingi wa Virusi mwilini ili kufikia lengo la 95-95-95

KAZI/ MAJUKUMU

- Kufanya vipimo vya kifua kikuu, vipimo vya wingi wa virusi mwilini na DBS (Damu kavu) na kuhakikisha zinahifadhiwa kwenye jotoridi na kuzisafirisha
- Kuweka kumbukumbu za huduma ya kifua kikuu, vipimo vya wingi wa damu na DBS na mfumo wa rufaa
- Kuweka kumbukumbu sahihi za wateja kwenye 'database'
- Kusambaza na kusafirisha majibu ya wingi wa virusi mwilini na DBS kutoka kituo kikuu (hub) kwenda vituo vidogo vinavyokusanya sampuli
- Kuandaa na kuwasilisha taarifa za sampuli za rufaa kwa mamlaka zinazohusika (CHMT,IP) kila mwezi
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na msimamizi wa maabara

SIFA, ELIMU NA UJUZI

- Awe mtaalam wa maabara aliyesajiliwa na mamlaka husika
- Awe na uzoefu wa kutumia mashine za maabara zinazotumia umeme na zisizotumia umeme
- Awe na uwezo wa kutumia kompyuta hususan 'Excel na database system'
- Awe na uwezo wa kufanya kazi mazingira aina tofauti
- Awe na leseni iliyohuishwa

- Awe na elimu ya cheti au stashahada ya sayansi ya maabara

II. Kazi: **Data Clerk (3)**

Eneo la kazi: **Handeni – Tanga**

Atawajibika kwa : **Mkuu wa kitengo cha huduma ya tiba na matunzo (CTC)**

MAELEZO YA KAZI

Data Clerk ataripoti kwa Mkuu wa kitengo cha huduma ya tiba na matunzo (CTC) na atapata ushirikiano kutoka kwa mratibu wa taarifa wa Halmashauri. Majukumu ya Data Clerk yatakuwa kama ifuatavyo:-

- Kuingiza taarifa sahihi za kitabibu, maabara, ufuatiliaji na vifaa vya uchambuzi yakinifu katika mfumo wa kielektroniki ikijumuisha taarifa za MTUHA.
- Kupitia taarifa za kwenye mfumo ili kuhakikisha kama ni sahihi na zimeingizwa kwa wakati
- Kuandaa orodha ya wateja ambao wanatarajiwa kuhudhuria kliniki na kuhakikisha mafaili yao yako sehemu sahihi na yanaweza kufikiwa na Tabibu.
- Kuandaa orodha ya wateja ambao hawajahudhuria kliniki kwa ajili ya kufanya ufuatiliaji baada ya kliniki
- Kuwasiliana na msimamizi kuhusu fomu zenye taarifa pungufu.
- Kupanga na kuweka fomu zinazohitajika kwenye mfumo wa namba au tarehe
- Kuwasiliana na msimamizi kuhusu matatizo ya 'database'
- Kufanya usuluhishi wa taarifa kati ya 'database' na vyanzo vingine vya taarifa kama rejesta na fomu za taarifa.
- Kutunza taarifa (soft and hard copies) na kuhakikisha zinapatikana kila zinapohitajika
- Kuhudhuria vikao vya kupitia na kuhakiki takwimu kwa wakati
- Kutoa ushauri kwa msimamizi juu ya kuboresha utunzaji wa takwimu
- Kufanya kazi nyingine zote zinazotokana na utoaji wa huduma

SIFA, ELIMU NA UJUZI

- Mwombaji awe na cheti au stashahada ya ujuzi wa kompyuta au taaluma inayofanana na hiyo. Wenye elimu zaidi watajiongezea sifa ya kuajiriwa.
- Ujuzi mzuri wa matumizi ya komputa hasa 'Microsoft access, excel, power point and word'
- Awe na uzoefu usiopungua mwaka 1 wa kuingiza taarifa kwenye mifumo mbalimbali
- Awe na kasi na umakini katika kuchapa
- Uwezo wa kufanya kazi kwa kujitegemea
- Mwenye uwezo wa kujieleza vizuri kwa kuongea na kimaandishi
- Anaefuata Sheria, Miongozo na Taratibu za kazi
- Mwenye uwezo wa kutunza siri
- Anayeweza kutatua matatizo, mshauri na mbunifu

III. Kazi: Mhudumu wa Afya Vijijini (Community Health Workers) (2)
Eneo la Kazi: **Handeni -Tanga**
Atawajibika kwa :**Mkuu wa kitengo cha huduma ya tiba na matunzo (CTC)**

KAZI/ MAJUKUMU

- Kusajili wateja kwa usahihi katika rejista au 'database' na kuwatambua wateja ambao hawajahudhuria kliniki au waliopotea.
- Kuchambua mafaili ya wateja waliopotea kutoka kwa afisa takwimu
- Kuwatafuta wateja kwa njia ya simu na kuweka kumbukumbu ya ufuatiliaji katika rejista
- Kuandaa mkakati wa kusaidia kuwatafuta wateja ambao hawapatikani kwenye simu kwa njia ya kuwafuata majumbani
- Kufuatilia wateja wa CTC/PMTCT/TB/HIV/ watoto na vijana waliopotea kwenye huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya na kuwarudisha kwenye huduma kwa asilimia 80.
- Kushirikiana na mtoa huduma anaehusika na rufaa na kuweka kumbukumbu sahihi za wateja wanaopata rufaa
- Kutafuta taarifa ya chanzo cha kifo cha mteja kutoka kwa ndugu mara kifo kinapotokea baada ya ufuatiliaji
- Kuhakikisha wateja wote waliopotea wamefuatiliwa ili kuwa na taarifa sahihi
- Kushirikiana na afisa takwimu ili kuhakikisha matokeo ya ufuatiliaji yamehuishwa katika "database".
- Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya ufuatiliaji ya siku, wiki na mwezi.
- Kusaidia kuainisha wagonjwa wa nje na vitengo vingine kwa ajili ya kupima na kubaini ndani ya kituo
- Kuandaa utaratibu wa kuwaunganisha wateja waliogundulika na maambukizi ndani ya kituo ili wapate huduma (LCM)
- Kusaidia kutoa elimu kwa wateja juu ya upimaji wa VVU kwa mteja, ndugu wa karibu na utayari wa kupata matibabu.
- Kuweka kumbukumbu ya taarifa zote kulingana na mifumo ya taarifa iliyowekwa.
- Kuhudhuria mafunzo yanayohusiana na huduma na matibabu ya UKIMWI
- Kufanya kazi zote utakazopangiwa na msimamizi wako.

SIFA

- Awe anajua kusoma na kuandika vizuri
- Awe na uelewa juu ya huduma za UKIMWI
- Mwenye utayari na uzoefu wa kufanya kazi na wenzie
- Mwaminifu katika jamii na kituo cha huduma
- Awe na Uzoefu uliothibitishwa wa kufanya kazi nyingine zisizohusiana na tiba

ELIMU NA UJUZI

- Awe na elimu ya kidato cha nne
- Mwenye cheti cha taaluma ya huduma za afya katika jamii (Community based health care) atapewa kipaumbele

IV. Kazi:Mshauri(Lay Councillor) (7)

Eneo la Kazi: **Handeni -Tanga**

Atawajibika kwa :**Mkuu wa kitengo cha huduma ya tiba na matunzo (CTC)**

KAZI NA MAJUKUMU

- Kutumia rejesta kutambua wateja ambao hawajahudhuria kliniki au waliopotea kwenye tiba
- Kuomba mafaili yaliyotambuliwa kama wateja waliopotea kutoka kwa afisa takwimu
- Kuwatafuta wateja kwa njia ya simu na kuweka kumbukumbu ya ufuatiliaji katika rejesta
- Kuandaa mkakati wa kusaidia kuwatafuta wateja ambao hawapatikani kwenye simu kwa njia ya kuwafata majumbani
- Kufuatilia wateja wa CTC/PMTCT/TB/HIV/ watoto na vijana waliopotea kwenye huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya na kuwarudisha kwenye huduma kwa asilimia 80.
- Kushirikiana na mtoa huduma anaehusika na rufaa na kuweka kumbukumbu sahihi za wateja wanaopata rufaa
- Kutafuta taarifa ya chanzo cha kifo cha mteja kutoka kwa ndugu mara kifo kinapotokea baada ya ufuatiliaji
- Kuhakikisha wateja wote waliopotea wamefuatiliwa ili kuwa na taarifa sahihi
- Kushirikiana na afisa takwimu ili kuhakikisha matokeo ya ufuatiliaji yamehuishwa katika "database".
- Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya ufuatiliaji ya siku, wiki na mwezi.
- Kusaidia kuainisha wagonjwa wa nje na vitengo vingine kwa ajili ya kupima na kubaini ndani ya kituo
- Kuandaa utaratibu wa kuwaunganisha wateja waliogundulika na maambukizi ndani ya kituo ili wapate huduma (LCM)
- Kusaidia kutoa elimu kwa wateja juu ya upimaji wa VVU kwa mteja na ndugu wa karibu na utayari wa kupata matibabu.
- Kuweka kumbukumbu ya taarifa zote kulingana na mifumo ya taarifa iliyowekwa.
- Kuhudhuria mafunzo yanayohusiana na huduma na matibabu ya UKIMWI
- Kufanya kazi zote utakazopangiwa na msimamizi wako.

SIFA

- Awe anajua kusoma na kuandika vizuri
- Awe na uelewa juu ya huduma za UKIMWI
- Mwenye utayari na uzoefu wa kufanya kazi na wenzie
- Mwaminifu katika jamii na kituo cha huduma
- Awe na Uzoefu uliohibitishwa wa kufanya kazi nyingine zisizohusiana na tiba

ELIMU NA UJUZI

- Awe na elimu ya kidato cha nne
- Mwenye cheti cha taaluma ya huduma za afya katika jamii (Community based health care) atapewa kipaumbele

V. Kazi:Tabibu (3)

Eneo la Kazi: **Handeni -Tanga**

Atawajibika kwa : **Mganga Mfawidhi wa Kituo**

1. KAZI NA MAJUKUMU

Kutoa huduma ya kliniki kwa PLHIV katika CTC pamoja na;

- Kutibu magonjwa nyemelezi
- Kutoa huduma katika kliniki ya wagonjwa wa VVU
- Kugawa dawa (ART) kwa wateja wapya waliotambuliwa (Uanzishwaji wa ART mara baada ya kutambuliwa)
- Aweze kutibu/ kushughulikia madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kupunguza makali ya Virusi vinavyosababisha UKIMWI(ARV)
- Kuanzisha na kufuatilia (post exposure prophylaxis)
- Kufuatilia wateja wanaotumia ART kwa kutumia mwongozo wa upimaji kitaifa (upimaji wa CD4, HVL, LFT na RFT)

2. Kutoa ushauri na matibabu kwa wagonjwa wenye VVU na waliopo wodini kama ikihitajika
3. Kutambua na kuanzishiwa IPT na MMS kwa wateja wanaostahili kupata
4. Kuhakikisha wateja wanahudhuria kliniki na kufuatilia wateja waliopotea kliniki
5. Kutunza taarifa sahihi za matibabu za wateja na kukusanya taarifa zingine mara kwa mara kwa ufuatiliaji na tathmini ya mipango, kuhakikisha ukusanywaji wa taarifa sahihi na wakati.
6. Kushiriki katika vikao (clinic – meetings) na kumsaidia msimamizi wake kuandaa na kusimamia mipango mkakati ya huduma
7. Kuratibu muunganiko wa huduma za CTC na HTS, STI, RCH, PMTCT, kliniki za kifua kikuu, IPD, FP, huduma za OPD, vikundi vya msaada wa PLHIV na programu za CBHS
8. Kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa wateja wenye VL ya juu kupitia ushauri nasaha

Majukumu mengine muhimu ya Tabibu.

- Kuwezesha mbinu za upimaji na kukabili VVU ikiwa ni pamoja na PITC iliyoimarishwa na upimaji wa ndugu wa karibu wa mteja (index testing) kulingana na mwongozo wa kitaifa wa VVU / UKIMWI / STI. Hasa anayehusika atasaidia katika uchunguzi wa wateja OPD kwa upimaji wa VVU, kuandaa index kwa mteja na ufuatiliaji wa anwani kwa ajili ya upimaji wa VVU.
- Kufanya kazi na wafanya kazi wengine wa kituo na washauri ili kuhakikisha utekelezwaji mzuri wa shughuli za usimamizi wa wateja wote wa VVU waliogunduliwa katika kituo
- Kutayarisha PITC, Usimamizi wa upimaji wa VVU kwa ndugu wa karibu na kutoa taarifa za upimaji za kila wiki na kila mwezi

SIFA, ELIMU NA UJUZI

- Awe na elimu ya stahhada(Diploma) ya utabibu
- Awe na uwezo wa kutumia kompyuta hususan 'Excel na database system'
- Awe na uwezo wa kufanya kazi mazingira aina tofauti

• VI. Kazi: Muuguzi (Enrolled Nurse)- (1)

- Eneo la Kazi: **Handeni -Tanga**
- Atawajibika kwa : **Mganga mfawidhi wa kituo**

1. KAZI NA MAJUKUMU

- Kutoa huduma katika kliniki ya wagonjwa wa VVU
 - Kugawa dawa (ART) kwa wateja wapya waliotambuliwa (Uanzishwaji wa ART mara baada ya kutambuliwa)
 - Kuanzisha na kufuatilia (post exposure prophylaxis)
 - Kufuatilia wateja wanaotumia ART kwa kutumia mwongozo wa upimaji kitaifa (upimaji wa CD4, HVL, LFT na RFT)
2. Kutoa ushauri na matibabu kwa wagonjwa wenye VVU na waliopo wodini kama ikihitajika
 3. Kutambua na kuanzishiwa IPT na MMS kwa wateja wanaostahili kupata
 4. Kuhakikisha wateja wanahudhuria kliniki na kufuatilia wateja waliopotea Kliniki
 5. Kutunza taarifa sahihi za matibabu za wateja na kukusanya taarifa zingine mara kwa mara kwa ufuatiliaji na tathmini ya mipango, kuhakikisha ukusanywaji wa taarifa sahihi na wakati.
 6. Kushiriki katika vikao (clinic – meetings) na kumsaidia msimamizi wake kuandaa na kusimamia mipango mkakati ya huduma
 7. Kuratibu muunganiko wa huduma za CTC na HTS, STI, RCH, PMTCT, Kliniki za kifua kikuu, IPD, FP, huduma za OPD, vikundi vya msaada wa PLHIV na programu za CBHS

8. Kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa wateja na wenye VL ya juu kupitia ushauri nasaha

SIFA, ELIMU NA UJUZI

- Awe elimu ya cheti cha uuguzi
- Awe na uwezo wa kutumia kompyuta hususan 'Excel na database system'
- Awe na uwezo wa kufanya kazi mazingira aina tofauti
- Awe na leseni iliyohuishwa

Majukumu mengine muhimu ya Wauguzi

- Kuwezesha mbinu za upimaji na kukabili VVU ikiwa ni pamoja na PITC iliyoimarishwa na upimaji wa index kulingana na mwongozo wa kitaifa wa VVU / UKIMWI / STI. Hasa anayehusika atasaidia katika uchunguzi wa wateja OPD kwa upimaji wa VVU, kuandaa index kwa mteja na ufuatiliaji wa anwani kwa ajili ya upimaji wa VVU.
- Kufanya kazi na wafanya kazi wengine wa kituo na washauri ili kuhakikisha utekelezwaji mzuri wa shughuli za usimamizi wa wateja wote wa VVU waliogunduliwa katika kituo
- Kutayarisha PITC, Usimamizi wa upimaji wa VVU kwa ndugu wa karibu na kutoa taarifa za upimaji za kila wiki na kila mwezi

- **VII. Kazi: Afisa Muuguzi Msaidizi (1)**
- Eneo la Kazi: **Handeni -Tanga**
- Atawajibika kwa : **Mganga Mfawidhi wa kituo**

1. KAZI NA MAJUKUMU

- Kutoa huduma katika kliniki ya wagonjwa wa VVU
 - Kugawa dawa (ART) kwa wateja wapya waliotambuliwa (Uanzishwaji wa ART mara baada ya kutambuliwa)
 - Kuanzisha na kufuatilia (post exposure prophylaxis)
 - Kufuatilia wateja wanaotumia ART kwa kutumia mwongozo wa upimaji kitaifa (upimaji wa CD4, HVL, LFT na RFT)
2. Kutoa ushauri na matibabu kwa wagonjwa wenye VVU na waliopo wadini kama ikihitajika
 3. Kutambua na kuanzishiwa IPT na MMS kwa wateja wanaostahili kupata
 4. Kuhakikisha wateja wanahudhuria kliniki na kufuatilia wateja waliopotea Kliniki

5. Kutunza taarifa sahihi za matibabu za wateja na kukusanya taarifa zingine mara kwa mara kwa ufuatiliaji na tathmini ya mipango, kuhakikisha ukusanywaji wa taarifa sahihi na wakati.
6. Kushiriki katika vikao vya kliniki na kumsaidia msimamizi wake kuandaa na kusimamia mipango mkakati ya kliniki
7. Kuratibu muunganiko wa huduma za CTC na HTS, STI, RCH, PMTCT, Kliniki za kifua kikuu, IPD, FP, huduma za OPD, vikundi vya msaada wa PLHIV na programu za CBHS
8. Kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa wateja na VL ya juu kupitia ushauri nasaha

SIFA, ELIMU NA UJUZI

- Awe elimu ya stashahada (Diploma) ya uuguzi
- Awe na uwezo wa kutumia kompyuta hususan 'Excel na database system'
- Awe na uwezo wa kufanya kazi mazingira aina tofauti
- Awe na leseni iliyohuishwa

Majukumu mengine muhimu ya Afisa Muuguzi Msaidizi

- Kuwezesha mbinu za upimaji na kukabili VVU ikiwa ni pamoja na PITC iliyoimarishwa na upimaji wa index kulingana na mwongozo wa kitaifa wa VVU / UKIMWI / STI. Hasa anayehusika atasaidia katika uchunguzi wa wateja OPD kwa upimaji wa VVU, kuandaa index kwa mteja na ufuatiliaji wa anwani kwa ajili ya upimaji wa VVU.
- Kufanya kazi na wafanya kazi wengine wa kituo na washauri ili kuhakikisha utekelezwaji mzuri wa shughuli za usimamizi wa wateja wote wa VVU waliogunduliwa katika kituo
- Kutayarisha PITC, Usimamizi wa upimaji wa VVU kwa ndugu wa karibu na kutoa taarifa za upimaji za kila wiki na kila mwezi

VIII. Kazi: Mteknolojia Dawa (Pharmaceutical Technologist) (Nafasi 1)

- Eneo la Kazi: **Handeni-Tanga**
- Atawajibika kwa: **Mganga Mfawidhi wa Kituo**

SIFA, ELIMU NA UJUZI.

Mwombaji awe umri kati ya miaka 18 hadi 41, Elimu kidato cha nne na kuendelea, Awe na Stashahada (Diploma) ya madawa kutoka katika chuo kilichosajiliwa na kutambuliwa na wizara ya Afya.


KAZI/MAJUKUMU YA MTEKNOLOJIA DAWA.

- Kugawa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa wanaoishi na V.V.U
- Kuhifadhi dawa na vifaa tiba kiusahihi na kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba.
- Kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya dawa

- Kukagua dawa, vifaa tiba kemikali vitendanishi na vipodozi.
- Kuanisha, kuandaa na kuagiza mahitaji ya dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi
- Kushiriki katika kazi zingine za kitengo cha dawa kituoni.

Kama umetimiza vigezo tajwa hapo juu unatakiwa uandike barua ya maombi ya kazi ukiambatanisha vyeti pamoja na wasifu binafsi (CV). Ikiwa umeajiriwa andika mwajiri wako wa sasa, anuani yake na nafasi unayoitumikia.

Barua zote zitumwe kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Handeni. **Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 20/09/2019.** Unaombwa kuandika namba yako ya simu chini ya saina yako ili iwe rahisi kufanya mawasiliano.


.....
Elizabeth Mwambashi
Kaimu Mkurugenzi
Halmashauri ya Mji
Handeni

**KRY:MKURUGENZI WA MJI
HANDENI**